Power Scholars Academy

Kwa ushirikiano na BELL (Building Educated Leaders for Life), Y na School District of Lancaster, Power Scholars Academy™ inatoa masomo ya majira ya joto kwa vijana wanaoingia daraja la 1-5. Lengo la mpango huu ni kuongeza mafanikio ya elimu ya wanafunzi, kukuza ujasiri na kushirikisha familia.

Mtoto wako ameteuliwa na shule yake na YMCA ili kupokea ufadhili wa masomo wa dola 1500 ili kuhudhuria Power Scholars kwenye Martin Elementary School. Ufadhili huu wa masomo unashughulikia gharama zote za mpango ikiwemo kifunguakinywa, chamcha, shughuli na ziara za nyanjani.

Power Scholars Academy hufanya kazi kuanzia **Jumatatu, tarehe 25 Juni – Ijumaa, tarehe 3 Agosti (hakuna vipindi wiki ya Julai tarehe 2)** kuanzia saa **8:00 asubuhi-3:00 alasiri**. Watoto wanahitajika kuhudhuria kila siku na kuingia bila kupitisha saa 8:15 asubuhi na kuondoka saa 3:00 alasiri.

Siku ya kawaida inajumuisha:

Wakati wa Jamii:
Wanafunzi, wanaoitwa wasomi, huanza siku kwa kifunguakinywa na shughuli ya wakati wa jamii ili kupata stadi za uongozi na urafiki thabiti na wasomi wengine na wafanyakazi.

Uwezo wa Kusoma na Kuandika:
Walimu walioidhinishwa wanaongoza mafunzo ya kusoma na kuandika kwa kutumia mtaala bora wa Scholastic. Mtaala unalenga stadi za kipaumbele ambazo ni muhimu kwa mafanikio ya wanafunzi: ufahamu wa fonimu, foni, ufasaha, misamiati na ufahamu.

Hisabati:
Walimu walioidhinishwa wanaongoza mafunzo ya hisabati kwa kutumia mtaala bora uliobuniwa na Scholastic. Mtaala unaangazia dhana msingi za kuwatayarisha wanafunzi kwa uelewa wa kina wa hisabati ya Common Core State Standards na umeundwa kama mpango wa ziada kwa ajili ya kuinua wasomi wa daraja la 1-5.

Chamcha na Mapumziko:
Wasomi hula chamcha na kutumia takribani dakika 30 kupumzika.

Ustawishaji:
Wasomi hupitia nafasi za ustawishaji wakati wa alasiri. Mada kwa kawaida hujumuisha Maendeleo ya Maisha na Uongozi, STEM, Afya na Ufaafu wa Mwili na Sanaa za Ubunifu (muziki, densi, sanaa).

Ziara za Nyanjani:
Kwenye Ijumaa zilizoteuliwa wasomi watahudhuria ziara ya nyanjani kando ya eneo.

Ikiwa ungependa kukubali ufadhili wa masomo wa mtoto wako kuhudhuria Power Scholars Academy

majira haya ya joto **jaza na urejeshe fomu ya usajili iliyoambatishwa kwenye shule yako bila kupitisha Jumatano, tarehe 28 Machi.** Hujahakikishiwa nafasi; mathibithso yatatumwa Aprili.

Tunatarajia kumwona mtoto wako majira haya ya joto!